# M A M L A K A

*Matayo Mt. 10:1 "Akawaita wanafunzi wake kumi na wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu, wawatoe na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina"*

*Nabii wa Mungu alivyosema juu ya hilo:*

Umbile letu la nje ni mtu mmoja; ndani yetu ni mtu mwingine. Kwa hiyo ndani yetu ni kitu cha kiroho; kwa nje yetu ni umbile linaloonekana. Unaona? Na utu huu, kama unaongozwa na Roho wa Mungu, unakuwa mjumbe wa Mungu au malaika. Mjumbe wa Mungu, Malaika wa Mungu ni neno hilo hilo; huwezi kuyatenganisha. Mjumbe wa Mungu au Malaika wa Mungu.

Ni yupi mwenye mamlaka kuu, malaika kutoka mbinguni au malaika aliyeko madhabahuni? Ni nani? Ni malaika aliyeko madhabahuni. Paulo alisema "kama malaika kutoka mbinguni atawahubiri ninyi Injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe. (2Kor. 12:4; 14 – 15, Galatia 1:6-10) kwa hiyo malaika aliye na upako wa Roho Mtakatifu na Neno anafuatia (ni wa pili) baada ya Mungu. (Hiyo ni kweli) katika mbingu, mamlaka yake ……..

Mamlaka yote mbinguni na duniani yako mkononi mwangu. "Basi enendeni, nami nipo pamoja nanyi (Matayo 28:18) Lolote mtakalolifunga duniani, nitalifunga mbinguni. Mtakalo lifungua duniani, nitalifungua mbinguni" (Matayo 16:18 – 19).

Oh kama Kanisa hili kubwa na takatifu lingetambua nguvu/uwezo wake wa kufanya mambo haya. Lakini kuna kutokuamini kwingi na woga na kutetemeka, kushangaa kama linawezekana, "Linaweza kutendeka"? Ili mradi hilo lipo, Kanisa kamwe halitaweza kusimama kwa usahihi. Na pale ambapo kila mazungumzo ya woga yatakapoondoka na Roho Mtakatifu achukue utawala wote wa Kanisa, hapo woga wote unaisha, na hilo kanisa lina nguvu. Unaona? Kwani wanacho nyuma yao kila kitu ambacho mbingu zinacho. Wao ni mabalozi wa kiti cha enzi. Hakika. Mabalozi wa Kristo wanayo mamlaka (2Kor.5:20), na kila kitu ambacho Kristo anacho ni chake Balozi. Naye akasema, "Enendeni ulimwenguni kote Roho Mtakatifu atakapokuja juu yenu mtakuwa mashahidi wangu" (Matendo 1:8). Na shahidi ni nini? Ni balozi, atakuja na kushuhudia kitu fulani. Nguvu zote za mbinguni ziko mikononi mwenu. Oh kwa nini tunakaa na Kanisa na halizai, na tumekaa hatuendelei? Ni kwa sababu hatutambui mambo haya.

Ninaogopa kwamba Kanisa halijui mamlaka yake. Ninaogopa ya kuwa watu waliozaliwa kwa Roho Mtakatifu hawajatambua mamlaka yao au Mamlaka ambayo Mungu ameyaruhusu katika Kanisa. Nitawapa ninyi funguo za ufalme. Chochote mtakachokifungua kitakuwa kimefunguliwa. Ninawapa mamlaka juu ya nyoka, na juu ya magonjwa yote, oh kila kitu, na hakuna kitu cha kuwadhuru (Marko 16:17 – 18). Ipe mazoezi imani yako. Iachilie. Mwache Mungu achukue njia yake. Mungu atakupatia hilo.

Mungu, Roho yule Mkuu, pale mwanzoni kabla hakujawa na mwanzo, Yeye alikuwa ni Mungu. Je ulijua ya kuwa ulikuwa ndani yake wakati huo? Kama wewe ni Mkristo ulikuwa ndani yake wakati huo. Na kama ni hivyo ilivyo, utu wote wa Mungu kwa jinsi ya mwili ukaumbika katika utu wa Yesu Kristo (Kolosai 2:9). Na ndipo Yesu alipokufa msalabani, nilikufa pamoja naye (Rumi 6:6; 2 Tim 2:11-13) kwa maana wakati huo nilikuwa ndani yake kwa maana alikuwa ni ukamilifu wa Neno lililodhihirishwa, kwa kujua kwamba tutadhihirishwa baadaye. Na tulikuwa msalabani pamoja Naye tulienda kaburini pamoja Naye, na tulifufuka pamoja Naye katika kufufuka. Na sasa tumepaa kwa Roho wake mpaka kwenye kiti cha Neema. Tukiketi pamoja na Kristo Yesu katika ulimwengu wa Roho (Efeso 2:4 – 6) siku zote.

Kama vile mbegu ya asili ya uhai inavyorithishwa, ikiwa imerutubishwa kutoka kwa baba, kadhalika maisha ya Kristo yamerutubishwa. Ndiyo maana Mungu anaitumia Roho ya Eliya mara tano tofauti. Ni nini? Ni kule kurithishwa.

Kama vile maisha yako ya asili na tabia zako zinavyorithishwa kutoka kwenye uzazi wa asili wa baba yako, kadhalika Roho wa Mungu aliyechaguliwa kimbele kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na pale ambapo Neno lote la Mungu liliumbika kwa ukamilifu ndani ya mwili wa binadamu aitwaye Yesu Kristo. Ndani hapo Mungu alinifanya nilipe kwa dhambi zangu ndani Yake. Ndipo akaniinua juu pamoja Naye katika kufufuka. Na sasa tumeketi pamoja naye tukiwa na Nguvu na mamlaka juu ya kila pepo. Oh kama tu unaweza kuamini kile Mungu alichotupa. Lakini kama hukuketi pale hutakuwa nayo. Na kama umeketi pale na huamini, na unaogopa kusogea, hutaweza kuitumia. Lakini kama umeketi pale, utaitumia kwa maana umekusudiwa kufanya unavyovifanya.

Hapa Yesu, kila kitu alichosema, Alinena tu Neno, nalo likawa hivyo (Marko 4:35-41). Mungu alimthibitisha kwamba ni Mwanae. "Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu ambaye nimependezwa naye. Msikieni Yeye"
(Matayo 17:1-8).

Mwangalie Yeye (nalipenda hilo) ni kwa ushujaa na kwa ukuu wa kifalme aliweza kusimama mbele ya waliomshutumu. Amina. "Alisema livunjeni hili hekalu, na nitamuomba Baba, na nione kile atakachofanya juu ya hilo". Livunjeni hili hekalu, nami nitalijenga – nitaliinua juu tena". (Yohana 2:19-22) Siyo. "Natumaini ku; nitaenda kujaribu ….. nitalifanya". Kwa nini? Maandiko yalisema hivyo. Maandiko hayo hayo yaliyosema ataufufua mwili wake, ndiyo yaliyotupa sisi mamlaka, Nguvu. Amina. "Katika Jina langu watatoa pepo; watanena kwa lugha ngeni; na kama wakishika nyoka au kunywa kitu cha kufisha; hakitawadhuru. "Kama wataweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya".

“Kwa nini unanililia mimi? Nena na uendelee mbele” Oh jinsi ilivyo ya kishujaa, “ I …. Livunjeni hili hekalu nitalijenga upya tena”.

Oh kumbukeni sasa ni Yeye yule yule; ni Yeye aliyesema katika (Yohana 14:12) “Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo, yeye atazifanya pia”. Hiyo ni kweli? Ni Yeye aliyesema hivyo. Ni Yesu katika Marko 11:24 aliyesema, “Kama utauambia mlima huu ‘Ng’oka’ na usione shaka moyoni, lakini waamini kwamba uliyosema yatatendeka, unaweza ukapata ulichosema”. Sasa kama unasema tu kwa kubahatisha, haitatokea; lakini kama kitu fulani ndani yako …… kwamba umepakwa mafuta kwa kazi hiyo, na unajua ni mapenzi ya Mungu kufanya hivyo, nawe utalisema, lazima litokee. Ni Yesu Kristo aliyesema hivi “kama mkikaa ndani Yangu na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni lolote mtakalo, nanyi mtapewa (Yohana 15:7).

Ninayo mamlaka ya kulitenda; lakini yanipasa nisubiri kupewa amri kulifanya. Unaona? Ninayo mamlaka kutoka kwa Mungu kulifanya, lakini sasa, pale anapotoa amri, ataenda nyumbani yu mzima unaona? Ninajua hiyo ni kweli.

Lakini kwanza, unaona, ni hayo yote …….. hakuna mmoja, hata Yesu mwenyewe alisema, Mwana hawezi kutenda neno kwa nafsi yake, lakini ni pale anapomuona Baba anafanya, hilo mwana naye hulitenda tunajua hilo (Yohana 5:19) sawa kabisa. Mwana hafanyi Neno lolote kwa nafsi yake, ila lile analomuona Baba akifanya, kadhalika Mwana hulifanya vile vile.

Mtu mmoja anasema “una nguvu?” Hakuna nguvu ndani ya mtu yeyote, lakini sisi kama waamini tunayo mamlaka, siyo nguvu. Hatuna nguvu za kutosha kufanya chochote.

Kama nilivyosema wakati uliopita, polisi mdogo hapa Louisville, akisimama pale. Yeye ni mdogo kuliko nilivyo mimi. Mtu mdogo dogo, kofia yake imevutwa chini mpaka maskioni mwake, na hii unifomu nusu ikining’inia nje yake anatembea nje kule barabarani, kofia ndogo pembeni mwake ifananayo na bastola, fimbo ndogo mkononi mwake, na filimbi ndogo. Anatembea pale akiwa na pea ya glovu nyeupe na yale magari (mengine ni hosi pawa mia tatu na hamsini) yalizunguka kule barabarani kama umeme. Yakinguruma zuum zuum, vyema, asingeweza kumsimamisha farasi mdogo anayekimbia katika nguvu zake, au hana nguvu zitoshazo kusimamisha baiskeli, hapana, hakika. Lakini alitembea nje kule barabarani, akiwa na beji kubwa inayong’aa, akipiga hiyo filimbi na kuinua mkono wake. Kama gari la hosi pawa miatatu linafunga breki na kila kitu chochote. Siyo nguvu za mtu, ni mamlaka aliyonayo. Ndivyo hivyo.

Hilo ndilo kanisa, linaweza likawa ni kundi la watakatifu wanaoviringika, jinsi wanavyoitwa au chochote unachotaka kuita; lakini ni yale mamlaka. Ni yale mamlaka nyuma ya hiyo; lakini ni yale mamlaka. Ni yale mamlaka nyuma ya hilo; hilo linafanya hivyo.

Bila kujali mazingira, sheria za Mungu zinatenda kazi na Neno. Sasa haitendi kazi na kanuni yako, itatenda kazi na Neno. Ndiyo, inatenda kazi pamoja na Neno hivyo tu. Sasa bila kujali hali (mazingira).

Sina nguvu zozote. Huna nguvu zozote. Lakini tunayo mamlaka (Amina). Ile beji ya imani inaning’inia kwenye Neno. Naamini hiyo ni kweli. Hicho ndicho kinachosimamisha. Hivyo unaweza kung’ang’ania.

Polisi mdogo anasimama nje pale akipuliza hiyo filimbi ndogo na kunyoosha mkono wake juu. Kila kitu kitaenda kusimama. Ni ile mamlaka yake ni ile mamlaka yake kuamini.

Hivyo kama mimi ni Mkristo na nimejazwa na Roho, nikiwa na ushuhuda wa Yesu Kristo aliyefufuka, kwamba Yeye ni yule yule, jana na leo na hata milele. Usiache shetani yoyote ajaribu kukusukuma hapo, kusema hufanyi hivi na”hufanyi vile” Kama unalifanya lifanye hilo. Mungu amekupa wewe…….. Unaona hatuna nguvu. Yule polisi hana nguvu za kusimamisha gari moja. Wakati mwingine ni hosi pawa mia tatu au mia nne. Angefanya nini juu ya hayo? Lakini anayo mamlaka.

Na hilo ni Kanisa, tunayo mamlaka, kwa kufufuka kwa Yesu Kristo na Neno lake la ahadi (Haleluya) kazi nifanyazo mtazifanya ninyi; kubwa kuliko hizi mtazifanya, kwa maana naenda kwa Baba (Yohana 14:12).

Yule askari wa Kirumi, kamanda wa mia, alishawishika kwamba kama tu angempata Yesu aseme Neno. Msikilize askari huyu, wa Kirumi, mmataifa, asiyejua Mungu. Akasema, sistahili wewe uje chini ya dari ya nyumba yangu. Sijihesabu mwenyewe hivyo. Lakini akasema, Mwanangu ni mgojwa sana na wewe unene Neno tu na mwanangu ataishi (Matayo 8:5 – 13); Luka 7:1-10) “Kwa maana mimi nimewekwa chini ya mamlaka nikimwambia mtu: Nenda hapa naye huenda, Na nikimwambia huyu mmoja njoo na anakuja” Kwa nini? Alikuwa na mamlaka juu yake. Alikuwa anashuhudia nini? “Yesu, Wewe u juu ya magonjwa yote, uko juu ya yote. Kama tu ningelikusikia wewe ukinena Neno, mtumishi wangu ataishi. Nimeshawishika kweli kweli. Ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni imani ya yule Mrumi. Aliliamini hilo.

Na Yesu alisema, “Nenda njia yako; mtoto wako anaishi” Yesu alisema hiyo ni Imani kubwa; hajaiona hiyo katika Israel “Nena Neno tu”.

Ilikuwa ni nini? Umbali haukufanya tofauti yeyote. Kwa sababu Mungu yuko kila mahali. Mungu ni asiyeshindwa na lolote. Na popote Mungu yupo, asiyeshindwa na kitu yuko popote. Na Mungu kwa kuwa Yeye yuko kila mahali, yamfanya Mungu awe mahali popote, juu ya yote. Unaona, Mungu ni mkuu katika Ujerumani, kule Switzerland na chini katika Africa. Katika saa hii Yeye yuko pale. Angalia hilo.

Na alichukua safari ya siku mbili. Na siku iliyofuatia kabla hajafika nyumbani, alikutana na watumishi wake wakimjia na wakamwambia “Mtoto wako anaishi”

Na Mroma (akida) huyu alisisimka mpaka akauliza ni saa ngapi alipoanza kuwa hajambo? Majira gani ya siku? Nao wakamwambia majira ya saa saba ndipo homa ilimwacha. Na Yule Akida (Mrumi) akafahamu ya kuwa ni saa ile ile aliyoambiwa na Yesu mwanao yu hai naye akawa ameamini. Amina.

Mwenye uwezo wote; aliye kila mahali, ajuaye yote Asiye na mwanzo wala mwisho, huyo ni Mungu.

Na kama ni Mwanamume au mwanamke, sijali hali gani unayo, unayo mamlaka kwa Ahadi ya Mungu, kwa sababu Yeye ni tajiri na ameahidi kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyawazayo (Efeso 3:20 – 21).

Nukuu za Kiingereza:
Maswali na majibu Waebrania sehemu ya 3 aya 631 – 634.“Mtazamo na nani ni Mungu” 50 – 0815, Mungu wa kizazi hiki kiovu Aya 67 – 69 Mbona unalia Nena Uk. 47. Maswali na majibu kitabu cha u.m.m. Uk 956. Kurudishwa kwa mti Bibi arusi Uk. 23. Kung’ang’ania (64-0619) kumuonea aibu Yeye uk. 34 kimo cha mtu mkamilifu uk. 19 – 20 shawishika na husika uk. 26 – 27 Mungu aliye mwingi wa Rehama Aya 147.

---

Jiwe la kujengea la kiroho no. 99. Kutoka Neno lililofunuliwa la saa hii. Yamekusanywa na: Gerd Rodewald, Friendenstr. 69, D-75328 Schomberg, Germany Phone: (+49) 72357613, Fax (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao utatoka moja kwa moja kwenye Biblia, na kazi ya haraka itaizunguka dunia, mbegu zitaandikwa magazetini, vitu vya kusomea mpaka kila mbegu ya Mungu iliyokusudiwa imesikia.
[Ndugu Branham Mwenendo – utaratibu – mafundisho uk. 724].

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*